

# Kausha pareto kwa kutumia miale ya jua ili kuongeza mapato



Karatasi ya nailoni juu ya trei



## Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

### Watayarishaji:

Wanjala N, Busienei TP na pertet EP

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Molo

S.L.P. 100, Molo

Simu: (051)721030/1, Nukulishi: (051) 721030

Baruapepe: nprckarimolo@yahoo.co.uk

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 75 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**



## Utangulizi

Ukaushaji ndiyo mojawapo wa matatizo yanayowakabili wakulima wa pareto humu nchini Kenya.

Teknolojia ya kukausha kwa kutumia miale ya jua imekuwepo humu nchini bila ya kutumika sana tangu mwaka wa 1999.

Ujenzi wa aina mbili za vifaa vya kukausha kwa kutumia miale ya jua umerahisishwa kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika maeneo yanayokuzwa pareto.

## Mtindo wa wakulima

Mtindo wa mkulima wa kawaida ni kukausha maua kwa kifaa fulani au kwa nchi kavu nje ya nyumba.

Mtindo huu husababisha kumwagika, kuchafuka, kuganda na hasara ya usafirishaji na uhifadhi.



**Kukausha pareto kwa karatasi ya nailoni**

## Mtambo wa kukausha kwa miale ya jua

Mjengo wa kukausha kwa kutumia miale ya jua unahusisha mihimili ya mbao inayowekelewa trei ambapo maua huwekwa.



**Trei juu ya mihimili ya mbao**

Mihimili hiyo ina nafasi ya kuwekelea karatasi ya nailoni ili kufunika pareto kunaponyesha na usiku pia.

Trei mpya za kahawa huwa zimeambatanisha na karatasi nyepesi ya nailoni inayotumika tu pindi kunaponyesha au usiku.

## Faida za vikaushaji vya jua

- Kukausha haraka na maua safi.
- Kupunguza upoteaji wa maua.

- Kupunguza kuganda na kiwango kizuri cha maua.
- Madini ya juu kwenye pareto na hivyo bei ya juu.
- Kupunguza kusambazwa na kuathiriwa na wanyama na hivyo kupunguza kupotea kwa pareto.
- Mkulima anaweza kufanya mambo mengi kwa pamoja.
- Kupunguza ulegevu na hata idadi ya wafanyi kazi.
- Inayofaa hasa wakati wa mvua kwa kutumia vipindi vichache vya jua vinavyopatikana.
- Inawezekana kwa urahisi maana rasilimali zinazohusika katika ujenzi hupatikana kwa urahisi katika maeneo hayo na ujenzi wake pia ni rahisi.

## Gharama

Maeneo tofauti tofauti yana changamoto zinazotofautiana au faida tofauti kuhusu rasilimali za ujenzi, hata hivyo mjengo mmoja hugarimu takriban shilingi 1,000 za Kenya.

Mjengo unaweza kuduma miaka 5 huku karatasi ya nailoni ikibadilishwa baada ya miezi 6 kwa gharama ya shilingi 180 za Kenya (Bei ya mwaka 2008).